# KCPE PREDICTION 2018

**PREDICTION PAPERS 2018** **KISWAHILI**

**INSHA:** Zilikuwa zimebaki siku chache ili kufanya mtihani wa kukamilisha darasa la nane. Nilikuwa nimejiandaa vya kutosha .....

**Soma vifungu vifuatayo. Vina nafasi 1 mpaka 15. Jaza kila pengo kwa jawabu lifaalo zaidi.**

Uamuzi ____1___ na serikali wa ____2___ watoto wote warudi shuleni ni jambo ___3____. Watoto walifurika ____4___ shuleni ili ____5___. Wale waliokuwa wakirandaranda mitaani ___6____ himahima na kupelekwa shuleni. Vitabu na sare __7_____ ili waanze masomo. Kwa miaka mingi ___8____ wazazi walishindwa kuwasomesha wana ____9___. Ama kweli walikuwa na furaha ____10___.

| | A | B | C | D |
|---|---|---|---|---|
| 1. | uliyofanywa | uliofanywa | ulifanywa | ulilofanywa |
| 2. | kuhimiza | kuwahimiza | kuwaapiza | kuwahamisha |
| 3. | mbora | njema | mwafaka | nzuri |
| 4. | pomoni | nomi | kochokocho | furifuri |
| 5. | kusahihisha | kusajiliwa | kusahilisha | kusajilishiwa |
| 6. | kufuatilizwa | ongoza | ongozana | fuatilisha |
| 7. | vilinunuliwa | kilinunuliwa | zilinunuliwa | ilinunuliwa |
| 8. | miongoni mwa | baadhi ya | badala ya | pachipachi mwa |
| 9. | wao | yao | wenu | wake |
| 10. | mingi | vingi | mwingi | nyingi |

Mtoto anastahili ___11____ kwa misingi ___12____ ya kinidhamu. Hoja ya wazazi ___13____ kujitafutia mali ___14____ kuwatambua warithi wa mali hayo ama kwa kweli ___15____.

| | A | B | C | D |
|---|---|---|---|---|
| 11. | kulewa | kulelewa | kuelewa | kulelea |
| 12. | dhabiti | dhalili | dhaifu | thabiti |
| 13. | isiwe tu | wasiwe tu | iwe tu | usiwe tu |
| 14. | mbali | mbari | bali | bari |

15. A. teke la kuku halimuumizi mwana
    B. chuma kiwahi kingali moto
    C. nazi ni tui la kwanza
    D. ukibebwa usilegeze miguu

**Kuanzia nambari la 16 hadi la 30 jibu kila swali kulingana na maelezo uliyopewa.**

16. Ni sentensi gani iliyo na kivumishi cha pekee.
    A. Mwanafunzi bora alituzwa na mwalimu.
    B. Milango mingi imetengenezwa na seremala.
    C. Miche hiyo itapandwa kesho.
    D. Kitabu kingine kilipotea jana.

17. Ni sehemu gani ya nazi inayotumiwa katika kuezeka?
    A. tui B. dafu C. makuti D. kifuu

18. Iandike sentensi ifuatayo katika hali ya wingi
    Mjomba na mkunga walivuliwa na mvuvi huyo
    A. Wajomba na wakunga walivuliwa na wavuvi hao
    B. Mijomba na mikunga walivuliwa na wavuvi hao
    C. Mjomba na mkunga walivuliwa na wavuvi wale
    D. Mijumba na mikunga walivuliwa na wavuvi hawa

**19.** Yapi si maana ya neno panda?
A. aina ya mnyama wa porini
B. paji la uso
C. bei kuongezeka
D. weka bima katika mashindano

**20.** Mchezo wa watoto wa kumfumba macho mtoto mmoja na kisha kutakiwa awatafute wenziwe huitwa?
A. Kibafute B. Bui
C. Gungwi D. Kodwa

**21.** Geuza sentensi ifuatayo katika usemi halisi
Mama alisema kwamba angepika pilau siku iliyofuata.
A. "Nitapika pilau siku ifuatayo," mama alisema.
B. "Nitapika pilau siku hiyo," mama alisema.
C. "Nitapika pilau kesho," mama alisema.
D. "Ningepika pilau siku ifuatayo," mama alisema.

**22.** Ni methali ipi yenye maelezo kuwa ukitaka kufanya jambo lichunguze na ulipime kwanza ili uelewe na ujue kitu utakachohitaji ili lifaulu
A. Nyumba njema si mlango fungua uingie ndani
B. Tahadhari kabla ya hatari
C. Sihadaike na rangi, tamu ya chai ni sukari
D. Gonga gogo usikie mlio wake.

**23.** Ni sentensi ipi inayoonyesha matumizi na wakati uliopo hali isiyodhihirika ?
A. Wanafunzi wanacheza kandanda
B. Juma naafute ubao
C. Chumba kimefagiliwa na mama
D. Nadurusu ili nipitie mtihani.

**24.** Tambua kiwakilishi katika sentensi ifuatayo.
Hicho kilichokuwa kikiwasumbua kimetatuliwa
A. Kilichokuwa B. Kimetatuliwa
C. Hicho D. Kikiwasumbua

**25.** Chumvi, sukari, unga, asali ni mfano wa?
A. Nomino fungamano B. Nomino za kawaida
C. Nomino dhahania D. Nomino za pekee.

**26.** Ni jibu lipi lenye kitenzi kutokana na sifa?
A. sana – msanii
B. sala – Sali
C. mpotevu – potea
D. uaminifu – aminika

**27.** Unga mweusi wa makaa au moshi ambao hupatikana kwenye sufuria au chungu cha kupika ni
A. mlale B. masizi
C. ukoko D. jivu

**28.** Ni sentensi gani iliyo na "ni" kuonyesha wingi?
A. Mkutano ulikuwa sebuleni.
B. Ni yupi aliyeadhibiwa na mwalimu?
C. Juma ni mwanafunzi mwema.
D. Waleteeni wageni vyakula wale.

**29.** Timu, jamaa, thureya, umayamaya yote ni
A. Nomino dhahania B. Nomino ambata
C. Nomino za makundi D. Nomino mahsusi

**30.** Kiungo kinachounganisha kiganja na sehemu ya juu ya mkono ni
A. Kitengele B. Kiwiko
C. Kisigino D. Kisugudi

**Soma habari ifuatayo kisha ujibu maswali 31-40.**

Tuliamshwa na kelele za mlango wa mbele ukivunjwa. Wakati huo huo roho yangu ilitaharuki. Mzizimo wa hofu ulinitambaa maungoni mwangu mithili ya sumu kali. Ghafla bin vu nilisikia mlango ukianguka chini kwa kishindo kikali. Muda wa koo kumeza punje ya nafaka, nilisikia mchakato wa nyayo ukielekea chumbani kwangu.

Kaka yangu wa toka nitoke alianza kulia machozi kwi kwi kwi. Nilishikwa na wayowayo na kutamani ardhi inimeze nikaikosa. Nywele zilinisimama kichwani, macho nayo, yakanitoka pima kama panya mtegoni. Jasho jembamba lilianza kunichururika.

Kufumba na kufumbua niliona upanga uliokuwa uking'aa. Ghafla kama ajali, mlango wa chumbani ulisukumwa na likaingia jitu lenye miraba miine na lililokuwa jeusi tititi. Nyuma lilifuatwa na genge la wenzake waliojihami kwa silaha tofauti tofauti.

Walipoingia waliniamuru kuwasha taa na kuufyata mdomo wangu ama sivyo wangalinichinja kaa kuku. Niliposikia hayo nilijikunja na kuanza kutetemeka. Baada ya kuvihamisha vyombo vyetu, walitufunga kifati na kutubeba hangahanga hadi nje kulikokuwa na giza totoro. Kabla ya sekunde kuunda dakika, majambazi hao walianza kunong'onezana na hapo nilimaizi kuwa huenda walikuwa wakila njama ya kutuangamiza.

Wazo hilo lilipobisha hodi taamulini mwangu mtima ulianza kunidunda kwa kasi. Niliyafumba macho na kuanza kusema sala kimoyomoyo. Ghafla bin vu, nilizinduliwa na sauti za halaiki ya watu waliojawa na mori. Nilifumbua macho na kushuhudia shani kadamnasi yangu. Shabash! Walikuwa ni majirani ambao walikuwa wamekuja kutuauni. Yakini heri jirani kuliko ndugu wa mbali na auni ni auni hakuna auni duni.

Wacha pazuke tandebelua! Katika kukuru kakara ile, majambaz i hao walizidiwa nguvu na wakaamua kusalimisha roho zao. Wakatundika miguu mabegani na kutoroka. Haooo! Wakachana mbuga. Hekaheka zilipotulia, majirani walitusaidia kuvirudisha virago vyetu mastakimuni. Niliwashukuru kwa kutuokoa katika jinywa la mauti.

31. Kelele za mlango zilimfanya mwandishi kuwa katika hali zifuatazo ila?
   A. kiherehere
   B. wayowayo
   C. hatihati
   D. ghadhabu

32. Mlango wa nyumba ulipovunjwa, ni yapi yaliyofuata?
   A. Wezi walijitoma ndani ya nyumba
   B. Mchakato wa nyayo za majambazi ulisikika kuelekea chumbani
   C. Kaka yake mwandishi alianza kulia kwi kwi kwi
   D. Mlango uling'oka na kuanguka

33. Si kweli kusema
   A. Majambazi walikuwa wamejihami
   B. Mwandishi na kakaye walilia kwa woga
   C. Aliyetangulia genge la wezi alikuwa bonge
   D. Mwandishi na kakaye hawakuwa pacha.

34. Genge la wezi lilitoa onyo lipi?
   A. Taa iwashwe mara moja
   B. Kutosonga wala kutotoka nje
   C. Kutosema be wala te
   D. Akina mwandishi kulala chini bila kusema lolote.

35. Ni nini maana ya "<u>.......... walitufunga kifati na kutubeba hangahanga?"</u>
   A. Walitufunga mikono na kutubeba juu juu
   B. Walitufunga mikono na miguu kisha kutubeba hobelahobela
   C. Walitufunga midomo na kutubeba hadi nje
   D. Walitufunga pamoja na kutubeba hobelahobela.

36. Unafikiria ni kwa nini genge hilo lilinong'onezana?
   A. Ili wasisike na watu kutoka nje
   B. Ili mwandishi na kakaye wasiwaone na kuwafahamu
   C. Ili wapange njama ya kuwaangamiza mwandishi na kakaye
   D. Ili maongezi yao yasijulikane na mwandishi

37. Mwandishi alikuwa katika hali gani halaiki ya watu ilipowasili?
   A. hali ya maombi na moyo kumpapa
   B. hali ya sala na jitimai
   C. hali ya wasiwasi na hoihoi
   D. hali ya kuomba na fedheha

38. Mwandishi anaposema kuwa ilikuwa ni shani kushuhudia halaiki ya watu ana maana gani?
   A. Hakuelewa jinsi ambavyo majirani walifika kwao
   B. Hakujua kiini hasa chao kuja huko
   C. Hakufahamu namna walivyopata habari kuhusu kuvamiwa
   D. Alifedheheka kuwaona watu waliofika nyumbani

39. Ni methali ipi inayofaa kuelezea kitendo cha wezi wale kukata kamba?
   A. Ushikawapo shikamana
   B. Kwa shujaa huenda kilio, kwa mwoga huenda kicheko
   C. Nia zikiwa moja kilicho mbali huja
   D. Hakuna marefu yasiyokuwa na ncha

40. Kichwa mwafaka cha habari hii ni?
   A. Uvamizi kitongojini.
   B. Maharamia wa kutisha.
   C. Majangiri wasio na huruma.
   D. Ujambazi ulioambulia patupu.

**<u>Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali 41 – 50.</u>**

Mihadarati ni dawa au tuseme ni vileo vinavyoathiri jinsi ambavyo waja hufikiria, huona hufanya na hata kuelewa mambo. Kwa kawaida waja huita mihadarati dawa za kulevya. Kila adinasi anafaa kujihadhari na kutotumia mihadarati la sivyo ataishia taabani.

Dawa za kelevya huathiri jamii hasa vijana ambao ni kama bendera ifuatayo upepo. Vileo kama vile ugimbi divai na baadhi ya mihadarati inayovutwa kama vilè tumbaku, bangi, heroini, madraksi.... orodha haishi. Kati ya mihadarati hii michache mno ndiyo haijaharamishwa nayo ni sigara na miraa.

Mihadarati huchangia pakubwa katika uenezaji wa maradhi, kunazo njia mbalimbali mojawapo ikiwa kutumia sirinji moja. UKIMWI umepata kupenya na kuzuka kama mizuka aushini mwa watu. Bila shaka janga hili limesafirisha wengi jongomeo kwa sababu wameyatemea mate mawaidha ya wakuu. Yamkini hasara humfika mwenye mabezo.

Uharifu nao umechipuka kama uyoga na kukita mizizi katika jamii. Mengi ya maovu yanayotendwa siku hizi ni kutokana na utumizi wa mihadarati wizi, ubakaji, uasherati, unyanganyi, ulawiti ni matendo yanayofanywa na watumiaji wa dawa za kulevya.

Aidha, wengi wa vijana wamerukwa na akili wamebaki kuzubaa ja mzungu wa reli. Hawaambiliki hawasemezeki. Hii ni hasara kwa uchumi wa nchi kwani taifa hupoteza watu wenye nguvu. Katika ndoa, mambo si tofauti utawasikia bibi na bwana wakirushiana chache za matusi mbele ya wanao. Ulevi wa mmoja wao huathiri familia. Kuikimu familia imekuwa ni shida, baba amekosa kuwajibika katika kuyakidhi maslahi ya familia yake kwa kufanywa ng'ombe wa shemere na ulevi.

Wanafunzi shuleni wameathirika pakubwa, wanaotumia dawa hizi wameyatupilia mbali masomo. Kwao kushika mkia si jambo la ibura. Wasichana nao wamejipata wamehimili. Haya yote yamesababishwa na utumiaji wa mihadarati, wengi wao wameshurutika kuacha masomo. Ama kweli mwangata mbili moja humponyoka.

Licha ya matatizo haya. Yapo mashirika ya kiserikali na yasiyo ya kiserikali yanayojikaza kisabuni kukabiliana na janga na jangamizi la mihadarati. Wote hawa wanaamini kuwa wataangamiza uraibu wa dawa hizi kwani baada ya dhiki ni faraja.

**41.** Kulingana na aya ya kwanza mihadarati ni
- A. dawa zinazoathiri namna mtu huona na kusikia mambo
- B. dawa zinazoathiri afya ya mtu kwa kumsababishia saratani tu
- C. dawa ambazo humlevya mtu na kusababisha talaka katika ndoa
- D. dawa zinazoathiri, kuvuruga na kubadilisha namna mwili unavyofanya kazi.

**42.** Ni kweli kusema
- A. mihadarati imeathiri vijana wote katika jamii
- B. mihadarati imeathiri vijana wanatetereka maishani
- C. mihadarati imeathiri vijana pekee katika jamii
- D. mihadarati imeathiri kila mtu katika jamii nzima

**43.** Ni mihadarati ipi kati ya hii imepigwa marufuku
- A. sigara
- B. miraa
- C. ugimbi
- D. heroini

**44.** Mwandishi ana maana yapi akisema
Uhalifu umechipuka kama uyoga na kukita mizizi
- A. uhalifu unaongezeka na kuenea kwa haraka sana
- B. uhalifu umeongezeka na kushitadi polepole
- C. uhalifu umeibuka na kutokomea katika jamii
- D. wizi na ubakaji umeongezeka sana.

**45.** Hasara kuu kwa uchumi wa nchi inayotolewa na mihadarati ni
- A. Kuvunjika kwa ndoa nyingi nchini
- B. Kuzidi kwa uhalifu nchini tu
- C. Kukosekana kwa wafanyikazi wenye rai
- D. Wanafunzi kutomaliza masomo yao shuleni.

**46.** Msemo kufanywa ng'ombe wa shemere umetumika kumaanisha
- A. kufushwa na ulevi
- B. kupotoshwa na ulevi
- C. kukamwa na ulevi
- D. kudhibitiwa na ulevi

**47.** Methali; Mwangata mbili moja humponyoka imetumika kurejelea
- A. wanafunzi kutumia mihadarati na kuwa wajawazito
- B. wanafunzi kutumia mihadarati na kupotea shuleni
- C. wanafunzi kutumia mihadarati na kufeli masomoni
- D. wanafunzi kutojali maisha yao ya halafu

**48.** Kulingana na mwandishi watu wengi wameambukizwa ukimwi kwa sababu gani?
- A. kupuuza mashauri
- B. kutumia sirinji moja
- C. kutemea mate wakuu
- D. kulimia mihadarati yote

**49.** Ni madhara mangapi yametajwa yanayoletwa na mihadarati?
- A. matano
- B. sita
- C. saba
- D. manane

**50.** Wanaonuia kuanza kutumia mihadarati wanastahili kutahadharishwa na methali gani
- A. Mla nawe hafi nawe ila mzaliwa nawe.
- B. Hakuna masika yasiyokua na mbu.
- C. Kupanda mchongoma kushuka ndio ngoma.
- D. Mtaka la waridi sharti adhurike.